LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website: www.humanrights.or.tz

for a Just and Equitable Society

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MWENENDO WA BUNGE LA KATIBA

TAREHE 17 SEPTEMBA 2014

Ndugu wanahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea kufuatilia kwa umakini na ukaribu mkubwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba mpya hususani hatua inayoendelea sasa ya Bunge Maalum la Katiba. Kwa nyakati tofauti tumeendelea kutoa mapendekezo kwa Bunge Maalum la Katiba kusitisha mijadala ya sura zilizosalia na kufanya kila liwezekanalo kumaliza mgogoro kati yao ili majadiliano yakiendelea kuwepo na uhakika wa kufikia kupiga kura ili Katiba mpya iwe na uhalali wa kisheria, kisiasa na kijamii

Ndugu wanahabari,

Kwa masikitiko makubwa mapendekezo hayo yamekuwa yakipingwa kwa maslahi ya kisiasa na kwa kauli zenye mrengo wa kuligawa Taifa na viongozi wenye dhamana kubwa ya kuwawakilisha watanzania kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Kwa mfano, mnamo tarehe 17/8/2014 Mwanasheria mkuu wa Tanzania, Jaji Frederick Werema alinukuliwa akisema;

> *'Rais Jakaya Kikwete hana mamlaka ya kulivunja Bunge Maalum la Katiba kwa madai ya kutokuwepo kipengele cha sheria'.*
>
> Ni wazi kauli hii haina maslahi wala uchungu kwa watanzania ambao ndiyo walipa kodi zinazowalipa posho wajumbe hao. Japo hakuna kifungu cha moja kwa moja kinachoeleza jinsi Bunge linavyoweza kuvunjwa, Bunge Maalum la Katiba limeteuliwa na Rais kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011. Sheria kifungu cha 22 kinaeleza kuwa Rais ndiye mwenye kuteua wajumbe wa Bunge hilo na nditye mwenye mamlaka akishauriana na Rais wa Zanzibar. Kifungu cha 22 (3) na (4). Kwa tafsiri ya kifungu hiki,

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

'Idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba watakuwa;

- *Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (357)*
- *Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (81)*
- *Wajumbe wa kundi maalum (201)'*

Vile vile kifungu cha 26 (2) Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, sura ya 83 toleo la mwaka 2012 kinasema;

'Ili Katiba inayopendekezwa iweze kupitishwa katika Bunge Maalum, itahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar.'

Kwa mujibu wa kifungu hiki kazi ya kujadili ibara/vifungu vya Rasimu ya Katiba inayofanyika sasa ni kupoteza muda kwani hatimaye itabidi kupiga kura ya kupitisha vifungu hivyo ili kupata Katiba inayopendekezwa. Jambo hilo haliwezi kufanikiwa kwasababu akidi ya theluthi mbili kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya kutoka Tanzania Zanzibar haiwezi kutimia.

Pia lazima tukumbuke kuwa katiba ni maridhiano.Maana ya maridhiano ni kuwa wote wanaohusika inabidi wawe pamoja katika kuipitisha katiba hiyo. Wasipoelewana hata kwa uchache tu maridhiano hayapo.Kwa hiyo hata ikilazimishwa na kupitishwa bado haitakuwa katiba ya wote na vuguvugu la kudai katiba litakuwa palepale baada ya kupoteza muda na fedha nyingi katika mchakato huu unaoendelezwa kimabavu.

Ndugu wanahahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimefanya uchambuzi ufuatao kuhusu akidi ya Bunge la Katiba.

Yafuatayo ni matakwa ya kisheria ya kutimia kwa Akidi katika Bunge Maalum la Katiba kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, ya mwaka 2011

1. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011

wajumbe wengi wa kutoka Zanzibar na Tanzania Bara hawahudhurii vikao vya Bunge maalum inavyoendelea kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Ndugu wanahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaendelea kusisitiza Bunge Maalum la Katiba liahirishwe sasa kuliko kusubiri tarehe 04/10/2014 litakapomaliza muda wake. Watanzania wanahitaji Katiba bora inayogusa maslahi yao, Katiba itakayopatikana kwa maridhiano baina ya pande zote na siyo kinachofanyika hivi sasa Bungeni.

Msimamo wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kuwa Suala la Uchaguzi halihusiani na Mchakato wa Katiba. Mchakato wa Katiba unaweza kabisa kuendelea na uchaguzi sambamba kwani Rasimu ya Katiba hususan **Ibara ya 268** inatoa kipindi cha mpito cha miaka minne kabla ya kuanza kutumia katiba mpya; hii ikiwemo na masuala ya uchaguzi na kutungwa kwa sheria mpya zitakazoendana na Katiba Mpya. Kusitisha mchakato kwa kisingizio cha uchaguzi ni kosa kubwa sana ambalo linatokana na kuwaachia wanasiasa mchakato huu. Wanasiasa kazi yao mara nyingi ni kuangalia maslahi ya kuwepo madarakani na kamwe si maslahi ya wananchi.

Ndugu wanahabari,

Kwa kuhitimisha Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinataka yafuatayo yatekelezeke;

i) Rais kwa nafasi aliyopewa kikatiba na katika Mchakato huu wa Katiba ana nguvu ya kuteua wajumbe wa bunge maalum la katiba achukue nafasi hii kuleta mwelekeo mpya juu ya mchakato wa katiba na hususani kusimamishwa kwa Bunge la Katiba na kuleta maridhiano ya mapungufu yaliyoonekana hapo awali yalio ondoa maridhiano hayo.

ii) Mwenyekiti wa Bunge la Katiba kusitisha mara moja vikao vyake ili muafaka upatikane kati ya pande mbili zinazokinzana. Kuendelea kuwa na vikao katika hali hii kutafanya Katiba inayoandikwa ikose uhalali wa kisiasa na kisheria ambao ni dosari kubwa kwa uandaaji wa Katiba

iii) Chaguzi za Serikali kuu na Serikali za Mitaa ziendelee kama ivyokuwa imepangwa kwa vile masuala haya mawili (Chaguzi na Mchakato wa Katiba) hayaingiliani kabisa kama ilivyoelezwa hapo awali.

iv) Wanasiasa waache mara moja kutoa kauli za kupotosha wananchi na zenye kebehi.